SHULE YA SEKONDARI EBENEZER – SANGO

PHONE +255 0732 972 908 ,0655 972 909
Reg: No. S. 4568, center No: S. 4901
E-mail: ebenezerac@yahoo.com
Website: WWW.ebenezerac.org

P.O. BOX 7703,
MOSHI.
TANZANIA.

PICHA

FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA KIDATO CHA 2015

A: YAHUSUYO MWANAFUNZI:-

1. Jina kamili……
2. Tarehe ya kuzaliwa……
3. Taifa……kabila……
   Mkoa ……wilaya……
   Dini……Dhehebu……..
4. Jinsia……..
5. Mahali unapoishi sasa hivi……

B: YAHUSU MZAZI /MLEZI

6. Jina la Baba Mzazi/Mlezi……
7. Anuani ya nyumbani……..
   Namba ya simu……..
8. Anuani ya kazini……
9. Kazi yake……
10. Jina la mama mzazi/mlezi……
11. Kazi ya mama/mlezi……..
12. Anuani yake……Simu……..
13. Anuani ya nyumbani ya mama/mlezi……

C: YAHUSUYO SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA

14. Jina la shule ya msingi ulipomaliza darasa la saba
    ……
15. Namba ya mtihani wa darasa la saba……
16. Mahali shule hiyo ilipo:
    Nchi……..Mkoa……..
    Wilaya……kata……
17. Mwaka ulipomaliza elimu ya msingi……..

D: **MAAGIZO MENGINE**

1. Malipo ya fomu ni shilingi elfu kumi (15,000), zinalipwa zote siku ya kuchukua fomu. Fedha za Fomu zikishalipwa hazirudishwi.
2. Mitihani ya usahili itafanyika tarehe ……., siku ya ……. saa mbili asubuhi hapa shuleni, Ebenezer Sango.
3. Mitihani itaanza saa mbili asubuhi hapa shuleni, Ebenezer -Sango.
4. Mwanafunzi afike akiwa na vifaa vya kufanyia mitihani mfano kalamu, rula, n.k.
5. Wanafunzi wote wavae sare zao za shule ya msingi.
6. Mwanafunzi afike akiwa na picha mbili ndogo. Pia mzazi ampatie fedha kidogo ya kununua chakula,n.k.

E: **MASOMO YA "O" LEVEL.**

7. Masomo yanayofundishwa katika shule ya E.S.S ni Civics, Basic Maths, Chemistry Physics, History, Geography , Biology, English language, Kiswahili, Bible Knowledge, Commerce, Book-keeping, Computer Literacy .
8. Umri wa mwanafunzi usizidi miaka kumi na tano (15), pia asiwe anayekariri kidato.
9. Tarehe ya mwisho ya kurudisha fomu zote shuleni ni ……
10. School Motto: "Soaring to greater heights"
11. Weka alama (v) katika lugha utakayotumia katika mtihani wa hisabati.

LUGHA YA KISWAHILI	**ENGLISH LANGUAGE**

Anuani ya barua pepe ya mzazi/mlezi (baba)…….
Anuani ya barua pepe ya mzazi/mlezi (mama)……
Anuani ya mwanafunzi……..

TANBIHI: Shule ina nafasi ya malazi kwa watoto wa kiume na kike.

Karibuni sana katika shule ya Sekondari Ebenezer-Sango kupata elimu bora na malezi.

School Motto: "Soaring to greater heights"

Ndimi katika utumishi,

……

Mkuu wa shule

SHULE YA SEKONDARI EBENEZER – SANGO

PHONE +255 0732 972 908
+255 0754 867 444
E-mail: ebenezerac@yahoo.com
Website: WWW.ebenezerac.org

P.O. BOX 7703,
MOSHI.
TANZANIA.

Ndugu ……

……

……

MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)

UTANGULIZI.

Tunayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule yetu kwa kidato cha kwanza kwa mwaka.

Shule itafunguliwa tarehe 06 Januari, 2014

Itakuwa siku ya Jumatatu. Wanafunzi wa bweni (boarding scholars) watatakiwa kufika shuleni tarehe 05/01/2014, saa 9 alasiri ili wapangiwe mabweni. Na endapo mwanafunzi hataripoti shuleni kwa kipindi cha majuma mawili (siku kumi na nne), nafasi yake itatolewa kwa mwanafunzi mwingine.

MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya Sekondari Ebenezer- Sango ipo katika kijiji cha Sango, kata ya Kimochi, karibu kabisa na Kimochi Sekondari, Mkoani Kilimanjaro. Kijiji cha Sango kipo umbali wa kama km8 kutoka Moshi Mjini barabara kuu ya Moshi-Dar Es-Salaam. Shule iko mkabala na kituo cha mafuta cha “Mount Meru” . uwapo mjini panda mabasi (Hiace) yaendayo Mjohoroni, au Holili kasha waambie wakushushie Mount Meru – Sango. Uwapo “Mount Meru petroleum Station” tazama kuelekea upande wa pili wa barabara utaiona shule ya Ebenezer Sango.

MASOMO YANAYOFUNDISHWA.

Yafuatayo ni masomo yanayofundishwa katika shule yetu: Historia(History), Jiografia(Geography), Kiingereza (English Language), Kiswahili, Uraia(Civics), Hisabati (Basic Mathematics), Fizikia (Physics), Kemia(Chemistry), baiolojia (Biology), Biashara(Commerce), Utunzaji hesabu (Book-keeping), Komputa(computer studies), elimu ya dini ya kikristo.

MAHITAJI YA MWANAFUNZI

(a) Mwanafunzi wa bweni:

- Kila mwanafunzi wa bweni atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:
- Godoro 6 x 2 ½ x 4 (urefu futi 6, upana futi 2 ½ na unene nchi 4)
- Blanketi 1 na mashuka mawili(2) , (wavulana bluu bahari, wasichana kijani nyepesi)
- Mto, foronya, taulo, chandarua na ngao.

- Beseni au ndoo ya plastiki, kandambili au mayeboyebo.
- Sanduku imara la kutunzia vifaa vyake lenye kufuli na begi la kubebea madaftari/vitabu darasani.
- Sabuni za kufulia, na kuogea (medicated soaps) za kutosha
- Nguo za ndani za kutosha.
- Mafuta ya kujipaka, dawa za mswaki, kiwi, brashi za kubrashia viatu, vitana.
- Karatasi za mitihani (rimu 2 kwa mwaka), kalamu za kutosha.
- Madaftari makubwa9quire 3 au 4) ya kutosha masomo yote, kalamu za wino (bluu/nyeusi) na risasi.
- Viatu vyeusi jozi mbili, vyenye kisigino kifupi vitakavyovaliwa pamoja na sare.
- Jozi mbili za soksi. Kwa wavulana soksi nyeupe na wasichana soksi nyeupe ndefu.
- Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set) na rula za kutosha.
- Picha ndogo za hivi karibuni (ukiwa umevaa shati jeupe).
- Nguo za michezo (bukta na fulana-jezi za Barcelona) kwa wavulana, wasichana bukta, sketi ya solo na fulana-jezi ya Barcelona.
- Viatu vya michezo (raba au njumu)

(b) Mwanafunzi wa Kutwa:

- Viatu vyeusi vya kamba, vyenye kisigino kifupi, vitakavyovaliwa na sare.
- Rimu mbili za karatasi (photocopying papers) kwa mwaka. 1 kwa muhula (miezi 6)
- Kalamu za wino (bluu/nyeusi) na za risasi za kutosha. Na mkebe wa vifaa vya hisabati
- Madaftari makubwa (3 quire or 4 quire) ya kutosha masomo yote.
- Biblia na vitabu vya nyimbo (wakristo)
- Soksi nyeupe kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.
- Nguo za michezo (bukta na fulana-jezi za Barcelona) kwa wavulana, wasichana bukta, sketi ya solo na fulana-jezi ya Barcelona.
- Viatu vya michezo (raba au njumu)
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko

MUHIMU: Vingi vya vifaa vilivyoorodheshwa hapo juu vinapatikana kwenye duka la shule kwa bei nafuu.
Dictionary (OXFORD ADVANCED LEARNERS)

SARE ZA WANAFUNZI

Sare zote za wanafunzi wa bweni na kutwa zitashonwa hapa shuleni . gharama itaonyeshwa kwenye kipengele cha ADA na malipo mengine.

Waama ni marufuku kwa mwanafunzi kurekebisha, kujinunulia au kujitengenezea, nje ya shule, sare na mavazi mengine yaliyoamriwa na shule.

FEDHA ZA MATUMIZI

Wazazi au walezi wanashauriwa kuwapa watoto wao fesha kiasi za matumizi kama vile kununua sabuni, kalamu, dawa ya meno, na kadhalika. Wanafunzi wote wanashauriwa kutunza fedha zao za matumizi katika ofisi ya keshia wa shule na siyo bwenini. Shule haitawajibika kwa vyovyote wala kuhusika na upotevu wa fedha

zitakazoibwa zikiwa bwenini kwa sababu yoyote. Aidha fedha za matumizi ZISITUMWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE. Zinaweza kutumwa kwa njia ya posta yaani kwa TMO au EMS au ziletwe moja kwa moja shuleni kwa keshia/msanifu wa shule.

SIMU YA MKONONI

Simu za mikononi haziruhusiwi kabisa hapa shuleni. Endapo mwanafunzi atakuwa na simu za mkononi hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake, zikiwemo kutaifishwa kwa simu hiyo pamoja na kusimamishwa masomo.

BAADHI YA SHERIA ZA SHULE

i. Mavazi rasmi ya shule yatavaliwa wakati wote ndani na nje ya shule. Pia mwanafunzi atavaa sare rasmi ya shule wakati wa kwenda nyumbani, kuja shuleni au kuripoti ofisini.
ii. Mwanafunzi atakayeshindwa kutimiza masharti yanayohusu mavazi ataadhibiwa vikali sana.
iii. Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni kama:
    (a) Kunywa au kulewa pombe
    (b) Kuvuta sigara, bangi au kutumia madawa ya kulevya
    (c) Kutoroka shule au kulala nje ya shule pasi na ruhusa ya shule
    (d) Kupigana au kupiga
    (e) Kufanya mapenzi shuleni au nje ya shule.
    (f) Kupata,kusababisha au kutoa mimba
    (g) Utovu wa nidhamu na kutomudu masomo
    (h) Kukosa kuhudhuria masomo kwa siku thalathini(30) au zaidi kwa mwaka bila sababu maalumu kama vile kuugua.
    (i) Kumgomea mwalimu adhabu au kukataa kutii sheria za shule.
    (j) Kuchochea mgomo, fujo au maandamano.
iv. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja shuleni na vifaa vya thamani kama vile redio kaseti, video, vitu vya thamani kubwa, mabegi, masanduku, magodoro, kamera, simu ya mkononi n.k.
v. Mawasiliano yote yaliyo rasmi baina ya mzazi/mlezi na shule sharti yapitie kwa mkuu wa shule. Ni marufuku kwa mzazi/mlezi kumwandikia mwanafunzi barua au kupiga simu akimwagiza mwanafunzi aombe ruhusa ya kuondoka shuleni.
vi. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutembelea majumba ya starehe, vilabu vya pombe au nyumba za kulala wageni. Aidha ni marufuku kutembelea nyumba za watumishi bila ruhusa maalum.
vii. Mapambo kama bangili, hereni, vidani, vikuku, mikufu ya shingoni, lip –stick, kunyoa kipara, rangi za kucha, kuchoma au kutia nywele dawa, kufuga kucha, kuvaa nguo fupi zilizopasuliwa au zinazoonyesha maumbile na kadhalika. HAZIRUHUSIWI SHULENI.
viii. Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na vyakula vya aina yoyote shuleni.
ix. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoa lugha chafu zisizofa, kama vile: matusi, maneno ya dharau na kebehi/kejeli kwa kutamka au kuandika dhidi ya uongozi wa shule, walimu, viranja, wafanyakazi wa shule za umma, wanafunzi wengine.
x. Ni marufuku kuharibu kwa makusudi samani, majengo au mali zozote za shule.
    Mzazi/mlezi atalazimika kufidia uharibifu wowote au gharama ya matengenezo.

Taswira ya Jumuiya ya shule ya Sekondari Ebenezer – Sango ni Elimu na malezi bora ya kikristo ya kukuwezesha kujitegemea. Tumia muda wako vizuri ili utimize maono yako ya maisha.

Tunakutakia maisha mema yenye mafanikio hapa Ebenezer- Sango Sekondari.

KARIBUNI SANA EBENEZER – SANGO SEKONDARI

…….